Toleo 94 - Rabi'al-thani 1446 H / Novemba 2024 M

# UQAB
Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Muozo wa Tabia na Maadili,Tunda la Mfumo wa Ubepari

**HABARI NA MAONI**
Mafunzo Baada ya Mwaka Mmoja wa Mauaji ya Halaiki Mjini Gaza

**MATOLEO**
Enyi Maulamaa Waheshimiwa! Simameni Imara Pamoja na Mashababu wa Hizb ut tahrir

**JIBU LA SWALI**
Dua Kwa ajili ya Kuangamizwa Umbile la Kiyahudi



Afisi ya Habari Kenya

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 03/1446 Jumatatu, 15 Rabi'al-thani 1446 H 18/10/2024 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Hizb ut Tahrir / Kenya Yafanya Mkutano na Waandishi wa Habari kuhusu Mwaka Mmoja wa Mauaji ya Halaiki dhidi ya Watu wa Gaza

Kufuatia kuendelea kwa mauaji ya watu wa Gaza yanayofanywa na umbile katili la Kiyahudi ambayo sasa yamepita mwaka mmoja, Hizb ut Tahrir/Kenya kupitia Afisi yake ya Habari ilifanya mkutano na waandishi wa habari mnamo siku ya Ijumaa, 18 Oktoba 2024. Mkutano huo na waandishi wa habari ulihudhuriwa na vyombo vya habari vinane nchini.

Katika mkutano huo na waandishi wa habari uliochukua takriban dakika 20, Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya, Ustadh Shabani Mwalimu alisisitiza mafunzo kadhaa ambayo Umma unapaswa kupata kutokana na mauaji yanayoendelea: maumbile ya ushujaa ya Waislamu huko Gaza, unafiki wa Baraza la Usalama na jumuiya nzima ya kimataifa miongoni mwa menngine yanayotolewa kutokana na mauaji hayo.

Hizb ut Tahrir / Kenya, ilikariri kuwa uvamizi wa kijeshi wa Wazayuni utaondolewa tu kwa ukombozi wa kijeshi. Na ukombozi wa Palestina kamwe hautakuja kupitia diplomasia au maazimio ya kimataifa. Majeshi ya Waislamu na watu wenye nguvu wana jukumu kubwa la kuwanusuru wana wa Ardhi Iliyobarikiwa - Palestina. Hizb ilito wito kwa Ummah kufanya kazi ya kusimamisha tena Khilafah kwa njia ya Utume ambayo itawakomboa na kuwaunganisha Waislamu, na kuregesha uadilifu, usalama, na heshima kwa wanadamu wote.

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir**

**Kenya**

# HABARI NA MAONI
# Mafunzo Baada ya Mwaka Mmoja wa Mauaji ya Halaiki Mjini Gaza

**Habari**:

Mwaka mzima umepita tangu tarehe 7 Oktoba 2023. Mwaka wenye mauaji ya halaiki na jinai zisizoelezeka dhidi ya Waislamu wa Palestina zinazoshuhudiwa na wote wenye macho ya kuona. Ni mafunzo gani tunaweza kupata tukitazama nyuma mwaka huu wa umwagaji damu na kutazamia mustakabali mwema kwa Palestina na Umma wa Kiislamu?

**Maoni:**

Mafunzo ya Ujasiri na Ustahamilivu kutoka kwa Waislamu wa Gaza

Waislamu wa Gaza wameonyesha nguvu na ustahamilivu mkubwa mbele ya ukandamizaji na ukatili usiokoma. Ujasiri wao ni ukumbusho kwetu sote maana ya kusimama kidete katika Imani na kumtegemea Mwenyezi Mungu, hata dhidi ya matatizo makubwa. Mapambano yao ya kila siku dhidi ya uvamizi wa Kizayuni, bila ya majeshi au usaidizi, yanaonyesha nia isiyoweza kuvunjika ya kupinga dhulma. Gaza imekuwa ishara ya nafsi ya Umma wa Kiislamu, ambayo haiwezi kupondwa kamwe, na itaendelea kuwa tayari kujitolea, mpaka ushindi ulioahidiwa wa Mwenyezi Mungu utakapopatikana. Zaidi ya hayo, Waislamu shupavu wa Gaza wamefichua kwa mara moja udhaifu wa uvamizi wa Kizayuni, ambao – licha ya ukatili wake wa kupindukia – unaendelea kutikiswa hadi msingi wake na upinzani kwa njia rahisi, na kamwe hautaweza kusimama kwa makabiliano na jeshi la kawaida la Waislamu.

Mafunzo ya Usaliti kutoka kwa Tawala katika Nchi za Waislamu

Tawala za nchi za Waislamu, bila ubaguzi, zimeiangusha Gaza na Palestina. Licha ya dhulma ya wazi, watawala katika ulimwengu wa Kiislamu wanaendelea na ushirikiano wao wa khiyana na ukaliaji kimabavu wa Kizayuni na utumwa wa Magharibi. Wametanguliza viti vyao vibovu vya utawala, utajiri wa duniani, na utumwa wa hila kwa mabwana zao wa kikoloni wa Magharibi kuliko kuwatetea wanyonge na wanaokandamizwa. Huku Al-Aqsa ikiendelea kukaliwa kimabavu, na Gaza inapigwa mabomu na njaa, wanaendelea kufunga mipaka na kutoa kauli tupu badala ya kutuma majeshi. Badala yake, baadhi yao walifungua mipaka ili kuruhusu tu vifaa kwa Wazayuni wauwaji wa halaiki, huku wengine wakionyesha uadui wa kisanii kwa Wazayuni, bila hatua zozote za kukomesha uvamizi huo au kuudhuru kwa njia yoyote thabiti; hivyo kuupa tu ujasiri kupanua jinai zake. Kufeli huku kunatokana tu na kutokuwa na nia, bali ni usaliti mwingine wa tena wa moja kwa moja wa Ummah, unaodhihirisha utiifu wa tawala hizi kwa maadui wa Uislamu.

Mafunzo Kuhusu Ulimwengu na Jumuiya ya Kimataifa

Jumuiya ya kimataifa kwa mara nyingine tena imejidhihirisha kuwa ganda tupu, linaloendeshwa na unafiki na undumakuwili. Huku wakidai kutetea haki za binadamu na uadilifu, mjini Gaza tunaona kwamba sheria zao zinatumika tu kulingana na matakwa ya kisiasa ya wenye nguvu, na msaada wao unaenea tu kwa wale wanaotumikia maslahi yao. Umoja wa Mataifa na taasisi nyingine za kimataifa zimekuwa zikishughulika vyema na kukaa kimya na kushiriki vibaya mno wakati mauaji ya halaiki yakiendelea na kupanuka. Hii inatufundisha kwamba ukombozi wa Palestina hautakuja kamwe kupitia diplomasia au maazimio ya kimataifa. Taasisi na maazimio haya sio kwamba hayafanyi kazi, badala yake, yalianzishwa kwa lengo hasa la kuhifadhi utawala wa wakoloni wa Magharibi, ambao kwao ukaliaji wa kimabavu wa Kizayuni ni mkono wake mwengine.

Uvamizi wa Kijeshi Utaisha kupitia Ukombozi wa Kijeshi

Historia na uhalisia wa sasa zinatufundisha kwamba uvamizi wa kijeshi wa Wazayuni unaweza tu kuondolewa kwa ukombozi wa kijeshi. Muhimu zaidi, hii ni amri ya Mwenyezi Mungu swt. Hakuna suluhisho jengine ambalo linakubalika Kiislamu au kimantiki. Gaza si janga la kibinadamu lisiloelezeka; ni sehemu ya vita dhidi ya Ummah. Uongozi wa Kiislamu pekee, Khilafah Rashida, ndio utakaovunja minyororo ya ukandamizaji na mgawanyiko wa kitaifa na kutuma majeshi kuikomboa Palestina yote. Jaribio lolote la kutafuta suluhu kwa njia ya mazungumzo na vikosi vinavyokalia kimabavu vitahusisha kusalimisha Ardhi Iliyobarikiwa ya Palestina, na kufanya usaliti dhidi ya Mwenyezi Mungu, Mtume Wake (saw) na Umma wa Kiislamu.

Mafunzo Kuhusu Sisi Wenyewe: Je, Tunasimama Wapi?

Ni lazima pia tujiangalie ndani na kujiuliza: Je, sisi kama Umma tunasimama wapi? Tunabeba jukumu la pamoja la kufanya kazi kwa ajili ya ukombozi wa Ummah na kusimamishwa kwa Uislamu kama mfumo kamili wa maisha. Gaza imefichua sio tu uzembe na kutoweza kwetu chini ya tawala za kisaliti za sasa, lakini pia uwezo wetu. Tunasimama kwenye njia panda ambapo ima tunaweza kuendelea kukubali kutawaliwa kwetu na utaratibu wa sasa wa kisiasa au tunaweza kufanya kazi ya kusimamisha tena Khilafah ambayo itawakomboa na kuwaunganisha Waislamu, na kuregesha haki, usalama na utu.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Elias Lamrabet**

# Enyi Maulamaa Waheshimiwa! Simameni Imara Pamoja na Mashababu wa Hizb ut Tahrir katika Mapambano ya Kuhuisha Uislamu kama Mfumo Kamili wa Maisha



Enyi Maulamaa waheshimiwa, Mwenyezi Mungu (swt) amekupandisheni hadhi kutokana na elimu ya Dini, kama Mwenyezi Mungu (swt) alivyosema ndani ya Quran Tukufu,

**[يَرۡفَعِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلۡعِلۡمَ دَرَجَٰتٖۚ وَٱللَّهُ بِمَا تَعۡمَلُونَ خَبِيرٞ]**

"Mwenyezi Mungu atawainua walio amini miongoni mwenu, na walio pewa ilimu daraja za juu. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda." [Surah Al-Mujadila 11]. Tunakuhutubieni kwa msingi wa hadhi hii iliyoinuliwa, kwani cheo cha juu huleta wajibu mkubwa zaidi. Tunakuhutubieni kwa matumaini na Dua kwamba sisi sote tunasimama miongoni mwa wanaosimamisha haki, na hatumuogopi yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu (swt).

Baada ya kuvunjwa Khilafah, matukio yaliyofuatana ambayo yalitokea katika karne iliyopita ya Hijri, na matokeo yake ya mwamko katika Ummah, yaliyozaliwa kutokana na imani ya Kiislamu (Aqida), ni dhahiri kwa kila mtu. Kuanzia mitandao ya kijamii hadi mikusanyiko ya kila siku, kurudi kwa utawala wa Uislamu imekuwa mada ya mjadala. Kutokana na kutojali na usaliti wa watawala wa Waislamu, mauaji yanayoendelea nchini Palestina yanayofanywa na umbile la Kiyahudi yamemlazimu kila Muislamu makini kutafakari juu ya ukombozi wa Ardhi hiyo Iliyobarikiwa, na njia za kuilinda dhidi ya uvamizi wa dola za Magharibi.

Katika hali hii, katika wadhifa wenu kama warithi wa Mitume (as), ni jukumu zito juu yenu kupaza sauti zenu kutoka misikitini, kuhusiana na kadhia ya uhai na kifo ambayo Umma wa Kiislamu unakabiliana nayo leo. Kadhia hii ni kusimamishwa kwa Khilafah Rashida kwa njia ya Utume, ambayo inalinda umoja wa Umma wa Kiislamu, nusra ya kijeshi kwa Waislamu wanaodhulumiwa, na kuanzishwa kwa mfumo wa kilimwengu wa Kiislamu.

Tunakuombeni kwamba katika kadhia hii, mutaungana nasi kuwalingania Waislamu wa Pakistan kuhusiana na masuala yafuatayo, bila kuogopa lawama za yeyote mwenye kulaumu mnaposema ukweli. Kama Mtume (saw) alivyosema,

**«لَتَأْمُرُنَّ بِالْمَعْرُوْفَ وَلَتَنْهَوُنَّ عَنِ الْمُنْكَرِ أَوْ لَيُسَلِّطَنَّ اللهُ عَلَيْكُمْ شِرَارَكُمَ. ثُمَّ يَدْعُوْ خِيَارُكُمْ فَلَا يُسْتَجَابُ لَكُمْ»**

"Lazima muamrishe mema na lazima mukataze maovu, au Mwenyezi Mungu atakusalitini kwa waovu wenu zaidi. Kisha walio bora miongoni mwenu wataomba, lakini dua zao hazitajibiwa." (Al-Tabarani katika Al-Mu'jam Al-Awsat).

**1.** Kutawala kwa mujibu wa amri zilizoteremshwa na Mwenyezi Mungu ni faradhi:

Mwenyezi Mungu (swt) amewajibisha Waislamu kwamba utawala wao lazima uwe juu ya maamrisho na makatazo ya Uislamu pekee. Katiba na sheria za dola yao lazima zivuliwe kwenye Shariah ambayo Mwenyezi Mungu (swt) aliiteremsha kwa Muhammad (saw). Hili linaweza kufikiwa tu pale dola ya Kiislamu, Khilafah, itakaposimamishwa. Mtawala, aliyeteuliwa kupitia Bay'ah ya utiifu ya Kisharia, anatekeleza Uislamu kwa watu, anatekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu katika mambo yote ya maisha, anaunganisha rasilimali za

***Endelea... UK 5***

Waislamu, na anaweka sera za kigeni kwa misingi ya Da'wah na jihadi. Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

[وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَا أَنزَلَ اللَّـهُ فَأُولَـٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ]

"Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio wapotofu." [Surah Al-Ma'idah: 47]. Mwenyezi Mungu (swt) ameteremsha,

[فَاحْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ وَلَا تَتَّبِعْ اَهْوَآءَهُمْ عَمَّا جَآءَكَ مِنَ الْحَقِّ]
"Basi hukumu baina yao kwa aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao ukaacha Haki iliyo kujia." [Surah Al-Ma'idah: 48].

Katika wadhifa wenu kama warithi wa Mitume, ni wajibu kwenu kuungana mikono na vijana (Mashababu) wa Hizb ut Tahrir ili kuwadhihirishia Waislamu wa Pakistan haja ya kuchukua kuubadilisha mfumo wa sasa wa demokrasia ya kisekula, kwa mfumo wa Mwenyezi Mungu (swt). Hili lazima lifanywe kwa namna ambayo wataiona kama jambo la kukatikiwa la uhai na kifo, na kujitolea wenyewe kwa mapambano ya kuendelea katika njia hii.

**2.** Kukataa Mfumo wa Kilimwengu, Ambao kwa Kweli ni Taghut, ni Faradhi
Mwenyezi Mungu (swt) ametuamrisha kukataa kila aina ya Taghut (batili au udhalimu). Mwenyezi Mungu (swt) asema,

[أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ آمَنُوا بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنْزِلَ مِنْ قَبْلِكَ يُرِيدُونَ أَنْ يَتَحَاكَمُوا إِلَى الطَّاغُوتِ وَقَدْ أُمِرُوا أَنْ يَكْفُرُوا بِهِ]

"Huwaoni wale wanao dai kwamba wameamini yale yaliyo teremshwa kwako na yaliyo teremshwa kabla yako? Wanataka wakahukumiwe kwa njia ya upotofu, na hali wameamrishwa wakatae hayo!" [Surah An-Nisa: 60].

Mtu yeyote au taasisi yoyote inayotunga sheria kinyume na amri zilizoteremshwa na Mwenyezi Mungu inachukuliwa kuwa ni Taghut. Watawala wa Pakistan kupeleka maamuzi kuhusu Waislamu kwa taasisi kama vile Umoja wa Mataifa, Baraza lake la Usalama, IMF, Benki ya Dunia, na FATF ni kitendo cha utiifu kwa Taghut. Ambapo Mwenyezi Mungu (swt) asema,

[وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ]

"Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni shetani (Taghut)'" [Surah An-Nahl: 36].

Katika wadhifa wenu kama warithi wa Mitume (as), lazima muungane mikono na vijana wa Hizb ut Tahrir katika kufikisha wito huu kwa Waislamu wa Pakistan: kwamba imani juu ya Mwenyezi Mungu, Muumba wa ulimwengu, inalazimu kukataa ukuu wa aina zote za ndani na nje za Taghut. Badala yake, ukuu wa sheria za Mwenyezi Mungu lazima usimamishwe kupitia mfumo wa Khilafah.

**3**. Kuvunja Masanamu ya Utaifa na Uzalendo ni Faradhi:

Fahamu za utaifa na uzalendo zilienezwa miongoni mwa Waislamu ili kuvunja umoja wa Ummah na kukata mshikamano wa udugu ambao umekita mizizi katika imani ya Kiislamu (Aqida). Fikra hizi zinawatenga Waislamu wanaoishi katika eneo moja na ndugu zao katika sehemu nyingine za dunia, hata kama makafiri wanawaua bila huruma watoto wa Kiislamu, wanawake na wazee katika maeneo hayo. Hata hivyo, Uislamu unaona kuwa mauaji yanayotokea Palestina sio tu wasiwasi wa watu wa Palestina pekee, ukandamizaji huko Kashmir sio kadhia ya watu wa Kashmir pekee, na vita vya wenyewe kwa wenyewe vinavyoendelea nchini Sudan sio tu tatizo la watu wa Sudan pekee, bali haya yote ni masuala ya Umma wa Kiislamu, na kuyatatua ni wajibu kwa Ummah mzima. Mwenyezi Mungu anasema,

[وَإِنِ اسْتَنصَرُوكُمْ فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمُ النَّصْرُ]
"Lakini wakiomba msaada kwenu katika Dini, basi ni juu yenu kuwasaidia." [Surah Al-Anfal: 72].

Utaifa na uzalendo ni aina za asabiyyah (ukabila). Kuhusu Asabiyyah, Mtume wetu kipenzi (saw) amesema:

«مَنْ قُتِلَ تَحْتَ رَايَةٍ عِمِّيَّةٍ يَدْعُو عَصَبِيَّةً أَوْ يَنْصُرُ عَصَبِيَّةً فَقِتْلَةٌ جَاهِلِيَّةٌ»

"Mwenye kuuwawa chini ya bendera ya watu vipofu, akilingania asabiyyah au kuunga mkono asabiyyah, kifo chake ni cha Kijahiliyyah (ujinga)" (Muslim). Utaifa na uzalendo ni fikra hatari. Kuzikumbatia kunapelekea kutelekeza faradhi ya jihad kwa ajili ya kueneza Uislamu kwa wanadamu wote.

Enyi watukufu maulamaa! Lazima muungane mikono na vijana wa Hizb ut Tahrir kufikisha amri ya Mwenyezi Mungu kwa Waislamu wa Pakistan, mpaka waache kila mwito wa 'asabiyyah. Ni lazima watambue kwamba hakuna Muislamu aliye bora au duni kwa kuzingatia utaifa wao, iwe Afghanistan au Pakistan au Palestina. Ni lazima pia waelewe kwamba majaribio ya kuwagawanya ni sehemu ya ajenda ya ukoloni, na kujitenga kwa Balochistan kutoka kwa Waislamu wengine, kutazidi kudhoofisha Umma. Fikra za ukuu wa rangi au kabila hugawanya Ummah, na kuimarisha mshiko wa makafiri juu ya Waislamu.

Ni wajibu kwenu kuangazia umbile la kimataifa la imani ya Kiislamu (Aqida) miongoni mwa Waislamu wa Pakistan, mpaka nyoyo zao ziunganishwe mbali zaidi ya kabila, rangi, lugha, na eneo. Ni lazima wahamasishwe ili kufuta mipaka bandia ya utaifa iliyochorwa kati ya ardhi za Waislamu.

4. Kukusanya Majeshi Kukomboa Ardhi Zinazokaliwa Kimabavu na Kutoa Nusrah (msaada wa kimada) kwa Waislamu Wanaokandamizwa ni Faradhi:

***Endelea... UK 6***

Hakuna aliye na haki ya kusalimisha sehemu yoyote ya ardhi ya Kiislamu, au kukubali utawala wa makafiri juu ya ardhi za Kiislamu, kwani Mwenyezi Mungu (swt) ameharamisha. Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

[وَلَنْ يَّجْعَلَ اللّٰـهُ لِلْكَافِـرِيْنَ عَلَى الْمُؤْمِنِيْنَ سَبِيْلًا]
“wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini.” [Surah An-Nisa: 141]. Uislamu unaamuru kwamba uvamizi wa makafiri ukomeshwe kwa nguvu za kijeshi, na kwamba wafukuzwe katika ardhi za Kiislamu. Mwenyezi Mungu (swt) asema,

[وَاَخْرِجُوْهُمْ مِّنْ حَيْثُ اَخْرَجُوْكُمْ]
“na muwatoe popote walipo kutoeni.”
[Surah Al-Baqarah: 191].

Ni wajibu kwa vikosi vya kijeshi vyenye uwezo na shujaa vya Pakistan kutumwa kuwasaidia Waislamu wanaodhulumiwa wa Gaza. Mwenyezi Mungu (swt) asema,

[وَمَا لَكُمْ لَا تُقَاتِلُوْنَ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَ الْمُسْتَضْعَفِيْنَ مِنَ الرِّجَالِ وَ النِّسَآءِ وَ الْوِلْدَانِ الَّذِيْنَ يَقُوْلُوْنَ رَبَّنَآ اَخْرِجْنَا مِنْ هٰذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ اَهْلُهَاۚ-وَ اجْعَلْ لَّنَا مِنْ لَّدُنْكَ وَلِيًّا وَّ اجْعَلْ لَّنَا مِنْ لَّدُنْكَ نَصِيْرًا]

“Na mna nini msipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanao onewa, wanaume na wanawake na watoto, ambao husema: Mola Mlezi wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhaalimu, na tujaalie tuwe na mlinzi anaye toka kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuru anaye toka kwako.” [Surah An-Nisa: 75]. Kuondoa kikwazo chochote kinachozuia kutekeleza faradhi hii pia ni faradhi, kama kanuni ya Sharia inavyosema, ما لا يتمُ الواجبُ إلا به فهو واجبٌ “Chochote ambapo wajibu hautekelezeki isipokuwa kwacho huwa hicho pia ni wajibu.”

Enyi Maulamaa waheshimiwa! Mnafahamu vyema kwamba kizuizi kikubwa kinachozuia majeshi kutekeleza wajibu huu ni watawala wa ardhi za Waislamu, ikiwemo Pakistan, ambao wamemfanyia khiyana Mwenyezi Mungu, Mtume wake (saw) na Umma kuhusu suala la Palestina. Enyi Maulamaa! Nyinyi ni warithi wa Maulamaa wakubwa kama Ibn Taymiyyah, Izz ad-Din Abd al-Salam, na Qadi Muhyi ad-Din Zaki, wakati wa uvamizi wa Matatari na Vita vya Msalaba, waliukumbusha Ummah wajibu wa Jihad na kuwawajibisha watawala. ili majeshi ya Waislamu yakusanywe kupigana na adui. Waliendelea kuhimiza majeshi na Ummah kuelekea jihad mpaka ardhi za Waislamu zikatwahirishwa kutokana na uchafu wa makafiri. Basi, ni nani miongoni mwenu atakayesimama kuwa mfuasi anayestahiki wa watangulizi wenu watukufu, ili vizazi vijavyo vikukumbukeni kwa heshima sawa na vile mnavyowakumbuka wale waliokuja kabla yenu?

**5**. Ni Faradhi Kusimamisha Utawala wa Uislamu Juu ya Dini Nyengine Zote:

Uislamu haukuteremshwa ili kuridhiana na dini nyingine au kuendeleza mifumo ya ukafiri. Badala yake, uliteremshwa ili kutawala dini nyingine zote, sheria, na mifumo ya maisha, na kuondoa batili. Mwenyezi Mungu (swt) asema,

[هُوَ الَّذِىْٓ اَرْسَلَ رَسُوْلَهٗ بِالْهُدٰى وَ دِيْنِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهٗ عَلَى الدِّيْنِ كُلِّهٖ وَ لَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُوْنَ]

“Yeye ndiye aliye mtuma Mtume wake kwa uwongofu na Dini ya Haki ipate kushinda dini zote, ijapo kuwa washirikina watachukia.” [Surah At-Tawbah: 33]. Leo, Uislamu utatawala tu mifumo mingine pale mfumo wa sasa wa kibepari wa dunia utakapobadilishwa na mfumo wa kilimwengu wa Kiislamu, jambo ambalo linawezekana tu kupitia kusimamishwa Khilafah kwa Njia ya Utume. Khilafah hii haikuegemezwa kwenye muundo wa dola za kitaifa, na sera yake ya mambo ya nje imejikita katika Da’wah (ulinganizi wa Uislamu) na Jihad. Pakistan, kwa sababu kadhaa, inafaa sana kuwa nukta ya nusra kwa ajili ya kusimamishwa kwa Dola ya Kiislamu.

Ni muhimu kwamba vijana wa Kiislamu wa leo wakumbushwe juu ya misheni waliokabidhiwa na Mtume wa mwisho (saw), na ukumbusho huu lazima utoke misikitini. Enyi Maulamaa, ni nani mwingine zaidi ya nyinyi anayeweza kutekeleza kazi hii muhimu? Enyi Maulamaa waheshimiwa, miaka mia moja iliyopita, makafiri Waingereza, kupitia kwa Mustafa Kemal, waliivunja Khilafah ya Waislamu. Hata hivyo, gurudumu la wakati limeregea kwenye nukta ile ile, na kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, karne hii wazi wazi ni ile ya mwamko wa Umma na Uislamu unaoinuka tena kama mfumo kamili wa maisha.

Wakati umefika wa sisi tuupe Ummah wetu ngao dhidi ya fikra na mifumo dhalimu iliyowekwa na makafiri. Wakati umefika sasa kwa sisi kuukomboa Umma wa Kiislamu, wakiwemo Waislamu wa Pakistan, kutoka kwenye udhalilifu na fedheha iliyowekwa na mfumo wa ulimwengu wa Magharibi kupitia kusimamisha tena Khilafah kwa Njia ya Utume. Huu ndio wakati wa kufanya kazi na watoto wa Ummah waaminifu na waadilifu, kutekeleza Shariah iliyobarikiwa ya Mwenyezi Mungu kwa kusimamisha Khilafah, na kuunganisha nguvu za Waislamu dhidi ya maadui zao makafiri, kurudisha heshima na utukufu wa Ummah. Wakati umefika sasa kwa Uislamu kuongoza ulimwengu na kuwakomboa wanadamu wote kutoka katika jinai na ukandamizaji wa mfumo wa kibepari.

**H. 8 Rabi' II 1446**
**M. : Ijumaa, 11 Oktoba 2024Hizb-ut-Tahrir**
**Wilayah Pakistan**

**JIBU LA SWALI**

# Dua Kwa ajili ya Kuangamizwa Umbile la Kiyahudi



**Swali:**

Assalamu Alaikum Wa Rahmatullahi Wa Barakatuhu Mwenyezi Mungu akulinde popote ulipo.

Nataka kukuuliza kuhusu ayah hii tukufu Mwenyezi Mungu Subhanahu Wa Ta'ala asema:

[وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِي إِذَا دَعَانِي فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ]

“Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anapo niomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi, ili wapate kuongoka.” [Al-Baqara: 186].

Je, ni kweli kwamba Mwenyezi Mungu hujibu dua zote za mwanadamu? Je, kuna dua ambayo Mwenyezi Mungu haijibu? Baadhi ya watu wanauliza, tumeombea Israel iangamizwe na Mwenyezi Mungu, lakini kwa nini umbile lao bado lina nguvu na linaendelea kuishambulia Gaza?

Shukran kwa jibu lako, Mwenyezi Mungu akulipe kheri kwa jibu lako zuri

Wassalamu Alaikum Wa Rahmatullahi Wa Barakatuhu

**Jibu:**

Assalam Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

Kuna mambo ambayo ni lazima yafahamike kuhusu Dua:

1- Iwapo Muumini atamuomba Mwenyezi Mungu kwa moyo wa ikhlasi, dua isiyokata kizazi, basi Mwenyezi Mungu (swt) atamjibu kwa njia moja kati ya tatu, kama ilivyo katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu (swt) na Sunnah za Mtume wake (saw):

Mwenyezi Mungu (swt) hujibu Dua ya muombaji anapomwomba, na humjibu mwenye haja anapomwomba;

[وَقَالَ رَبُّكُمُ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ]

“Na Mola wenu Mlezi anasema: Niombeni nitakuitikieni.” [Ghafir: 60]

[وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ]

“Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anapo niomba.” [Al-Baqara: 186]

[أَمَّنْ يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكْشِفُ السُّوءَ]

“Au nani yule anaye mjibu mwenye shida pale anapo mwomba, na akaiondoa dhiki” [An-Naml: 62].

Hata hivyo, jibu lina uhalisia wa Shariah ambao ulielezwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw):

«مَا مِنْ مُسْلِمٍ يَدْعُو اللهَ عَزَّ وَجَلَّ بِدَعْوَةٍ لَيْسَ فِيهَا إِثْمٌ وَلَا قَطِيعَةُ رَحِمٍ، إِلَّا أَعْطَاهُ اللَّهُ بِهَا إِحْدَى ثَلَاثِ خِصَالٍ: إِمَّا أَنْ يُعَجِّلَ لَهُ دَعْوَتَهُ، وَإِمَّا أَنْ يَدَّخِرَهَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ، وَإِمَّا أَنْ يَصْرِفَ عَنْهُ مِنَ السُّوءِ مِثْلَهَا». قَالُوا: إِذًا نُكْثِرُ. قَالَ: «اللَّهُ أَكْثَرُ»

“Hakuna Muislamu yeyote atakayeomba dua isiyokuwa na uovu ndani yake wala isiyokata kizazi isipokuwa Mwenyezi Mungu atampa moja katika mambo matatu: Atamjibu haraka dua yake, au atamwekea kesho Akhera, au amuepushie kiasi sawa cha uovu.”

*Endelea... UK 8*

Wale waliosikia wakasema wataomba dua nyingi na akajibu kuwa Mwenyezi Mungu yuko tayari zaidi kujibu kuliko wanavyoweza kuomba.” (Imepokewa na Ahmad 3/18).

Pia,

**«لَا يَزَالُ يُسْتَجَابُ لِلْعَبْدِ مَا لَمْ يَدْعُ بِإِثْمٍ أَوْ قَطِيعَةِ رَحِمٍ مَا لَمْ يَسْتَعْجِلْ». قِيلَ: يَا رَسُولَ اللهِ، مَا الِاسْتِعْجَالُ؟ قَالَ: «يَقُولُ قَدْ دَعَوْتُ وَقَدْ دَعَوْتُ فَلَمْ أَرَ يَسْتَجِيبُ لِي فَيَسْتَحْسِرُ عِنْدَ ذَلِكَ وَيَدَعُ الدُّعَاءَ»**

“Mja hataacha kujibiwa kwa sharti kwamba haombi chochote cha dhambi au kukata kizazi, na maadamu hana pupa. Alipoulizwa ni nini maana ya kuwa na pupa, Mtume wa Mwenyezi Mungu alijibu: “Ni pale anaposema kwamba ameomba na kuomba lakini sijibiwi, basi basi akachoka katika hali hiyo na kuacha dua.” (Imesimuliwa na Muslim 4918).

Tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) na tukiwa wakweli, waaminifu, na watiifu, basi tuna yakini na jawabu kwa namna alivyoeleza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw).

2- Dua sio njia ya Shariah ya kufikia lengo katika hali zote... Inapendekezwa, lakini sio njia ya kupata ushindi katika vita au kusimamisha dola nk. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alitayarisha jeshi huko Badr na kuwapanga askari, kila mmoja kwa nafasi yake, na akawatayarisha vyema kwa ajili ya vita, kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akaingia kwenye hema, na akamuomba Mwenyezi Mungu apate ushindi, na akazidisha dua mpaka Abu Bakr, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, akamwambia: “Baadhi ya haya yanakutosha ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.” (Sirat Ibn Hisham 2/626). Dua haimaanishi kuacha kuchukua njia zinazohitajika, bali ni sehemu muhimu yake.

Pia anayetaka Khilafah isimamishwe tena, asitosheke na kumuomba Mola wake ili kufanikisha hilo, bali ashirikiane na watenda kazi ili kuisimamisha na kumuomba Mwenyezi Mungu msaada katika hilo, na kuliharakisha kufanikiwa, na dumu katika kumuomba Mwenyezi Mungu kwa ikhlasi huku ukichukua njia zinazohitajika. Hivyo, katika matendo yote, mtu anatakiwa kuwa na ikhlasi katika kitendo kwa Mwenyezi Mungu na awe mkweli kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) na aombe dua na kudumu katika kuomba, na Mwenyezi Mungu ni Samiy’ Mujeeb (Mwenye kusikia na Mwenye kujibu).

3- Siku za nyuma tulijibu swali kama hili mnamo tarehe 4 Dhul-Qi'dah 1432 H - 1/10/2011 M, na linasema:

[...Ama dua huku ukichukua njia zinazohitajika, ina athari katika matokeo, na hivi ndivyo alivyofanya Mtume (saw) na walivyofanya maswahaba zake. Mtume (saw) alilitayarisha jeshi na akaingia kwenye hema kuomba dua. Waislamu katika Al-Qadisiyah walijitayarisha kuuvamia mto. Sa'd, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, alielekea kwa Mwenyezi Mungu kwa dua...Na hivyo waumini wenye ikhlasi hujitayarisha kimada na kuomba dua. Mwenye kutafuta riziki hujitahidi huku akiomba dua, na mwanafunzi husoma na kujitahidi huku akimuomba Mwenyezi Mungu ili afanikiwe. Hili lina athari katika matokeo, Mwenyezi Mungu akipenda.

Imeelezwa katika “Mafahim” (Fahamu za Hizb ut Tahrir) mwishoni mwa ukurasa wa 50: “Lazima ifahamike kwamba ingawa kitendo kilichoashiriwa na Tariqah ni kitendo cha kimada (maadiyyah), ambacho kinapata matokeo ya kuhisika (mahsuusa), kitendo hiki lazima kiende kwa kufuata maamrisho (awaamir) na makatazo (nawaahi) ya Mwenyezi Mungu (swt). Kufuata maamrisho na makatazo ni kwa ajili ya radhi (riDwaan) ya Mwenyezi Mungu (swt). Muislamu pia lazima atawaliwe na utambuzi wake wa uhusiano wake na Mwenyezi Mungu (swt), ili atafute ukaribu (qurbah) na Mwenyezi Mungu (swt) kupitia Swalah, Dua, kisomo (tilawah) cha Quran na kadhalika. Ni lazima pia aamini kwamba Nasr (ushindi) unatoka kwa Mwenyezi Mungu (swt). Ni lazima taqwa (uchamungu) iwekwe katika nyoyo ili kutekeleza hukmu za Mwenyezi Mungu (swt). Pia ni muhimu kuomba Dua na kumdhukuru Mwenyezi Mungu (swt), huku tukidumisha uhusiano na Mwenyezi Mungu (swt), wakati wa kufanya vitendo vyote.”

Ni wazi kutokana na hili kwamba umuhimu wa dua kuambatanishwa na kuchukua njia zinazohitajika katika matendo yote ya muumini. Umuhimu huu unaongezeka kwa kurudiwa kwa neno “ni lazima” kuashiria umuhimu mkubwa kwamba vitendo vyote viambatanishwe na dua na mwendelezo wa kushikamana na Mwenyezi Mungu ...

- Utumiaji wa dua pamoja na kuchukua njia za lazima ni kama tulivyosema, aliyoyasema Mtume (saw) na Maswahaba zake, na Waumini walikuwa juu yake, na ikiwa yataunganishwa basi yanakuwa na athari juu ya matokeo, Mwenyezi Mungu akipenda. Utumiaji wao kwa pamoja haugongani na njia ya Uislamu, bali kinachogongana nayo ni kujifunga na dua peke yake bila ya njia ambayo nususi zimeonyesha katika utekelezaji fikra ya Kiislamu...]

Kwa hivyo, yaliliyotajwa katika swali lako kuhusu dua ya kuondolewa kwa umbile la Kiyahudi... dua haitoshi kwa hili, bali kitendo cha jeshi la dola linalopigana na Mayahudi lazima kiambatane na dua, kama ilivyokuwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) na Maswahaba zake, Mwenyezi Mungu awe radhi nao. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye msaada.

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**4 Rabi’ Al-Akhir 1446 H**

**7/10/2024 M**